**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YAWIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NAMAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
Dodoma

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018]*

**APRILI, 2018**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi 2018. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29 Machi, 2018 ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ina Mafungu 8 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,

iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,

v) **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama,

vi) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,

vii) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na

viii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita na Wilayani Chato, kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2018. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini inayosimamiwa na Wizara ya Katiba kupitia Mahakama. Taarifa kuhusu yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi pamoja na Ushauri wa Kamati kwa kila mradi ni kama inavyoainishwa katika Jedwali lifuatalo (Jedwali Na.1).

## JEDWALI NA.1: REJESTA YA TAARIFA KUHUSU MIRADI YA UJENZI WA MAHAKAMA ILIYOKAGULIWA NA KAMATI

| Na. | **Namba na Maelezo ya Mradi** | **Mamlaka inayotekeleza Mradi** | **Thamani ya Mradi** | **Mahali unapotekelezwa** | **Tarehe ya Kuanza Mradi (As per plan) na Muda tarajiwa wa Mradi** | **Kiasi cha Pesa kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018** | **Kiasi kilichotolewa mpaka kufikia wakati wa ziara** | **Hali ya Mradi wakati wa ziara** | **Maoni ya Kamati kuhusu hatua ya Mradi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Mradi Na.6314** Ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga | Mahakama ya Tanzania **FUNGU 40** | **Bil.4.4** | Manispaa ya Shinyanga | Awamu tatu: 2006/2007, 2011/2012 na 2014-2017 | - | **Bil.4.4** | Ujenzi umekamilika | Utekelezaji wa Mradi ni wa kuridhisha |
| 2. | **Mradi Na.6310** Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Geita*(Resident Magistrate Court) kwa teknolojia ya ghrama nafuu ya Moladi* | Mahakama ya Tanzania **FUNGU** 40 | Mil.644.40 | Mkoani Geita | 2017/2018 | Mil.644.40 | Mil.120.04 | Ujenzi wa msingi upo katika hatua za Mwisho | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |
| 3. | ***Mradi Na.6310*** *Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Simiyu(Resident Magistrate Court) kwa teknolojia ya gharama nafuu ya Moladi* | Mahakama ya Tanzania **FUNGU 40** | Mil.644.38 | Mjini Bariadi | 2017/2018 | Mil.644.38 | Mil.198.88 | Ujenzi wa Msingi umekamilika | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |
| 4. | ***Mradi Na.6310*** *Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Chato kwa teknolojia ya gharama nafuu ya Moladi.* | Mahakama ya Tanzania (FUNGU 40 | Mil.644.38 | Wiayani Chato | 2017/2018 | Mil.644.38 | Mil.198.32 | Ujenzi wa Msingi umekamilika | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukaguzi wa Miradi husika hapo juu, pia Kamati ilipokea taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa chini ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo imetengwa katika makundi manne. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;-

i) **Mradi Na.6310** - Kujenga na Kukarabati Majengo ya Mahakama za Wilaya za Ngorongoro, Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Geita, Bariadi, Bukombe, Chato, Kondoa, Longido, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Lindi, Mpanda, Rungwe, Bunda, Kilindi, Kasulu na Sikonge.

ii) **Mradi Na.6312 -** Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo za Kawe, Karatu, Old Korogwe, Wasso - Loliondo, Totowe, Magoma - Korogwe, Robanda - Serengeti, Itinje - Meatu, Iguguno - Singida, Bareko - Kondoa na kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mwazo Mvomero - Morogoro.

iii) **Mradi Na.6314**: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo za Mahakama Kuu Kigoma, Mara na kukarabati Mahakama Kuu Sumbawanga.

iv) **Mradi Na.6391:** Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Majaji nchini (Ukarabati wa Makazi ya Jaji Mkuu, Nyumba za kufikia Majaji za Mtwara, Kigoma na Musoma).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya tarehe 19 Machi, 2018, Mahakama imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Majengo Matano(5) kwa ujenzi wa kutumia teknolojia ya gharama nafuu (MOLADI) ambayo ni Mahakama za Wilaya ya Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama ya Mwanzo Kawe.

Aidha, Mahakama imekamilisha Miradi mingine Minane (8) ambayo ilikuwa imekwama katika hatua mbalimbali katika kipindi cha nyuma. Miradi hiyo ni Mahakama za Mwanzo Karatu (Arusha), Loliondo (Ngorongoro), Robanda (Serengeti) na Totowe (Songwe).Ujenzi ulioko katika hatua za mwisho ni pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara na Mahakama za Mwanzo za Magoma (Korogwe) na Itinje (Simiyu).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki. Hata hivyo, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka Paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya Sehemu za Paa hilo wakati bado Jengo ni jipya na hivyo kuhitaji ukarabati wa haraka. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kuokoa athari zinazoweza kujitokeza kwa Jengo ambalo limegharimu mabilioni ya fedha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango

ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa Fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

## 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano Saba Elfu na Mia Mbili (24,087,507,200/=).** Hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tisa Sitini na Saba, Laki Nane Arobaini na Moja Elfu, Mia Moja Sitini na Nne (12, 967,841, 164)** sawa na **asilimia 54** ya lengo lililokusudiwa.

## 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tatu, Milioni Mia Mbili Arobaini na Tatu na Sabini na Nane Elfu (143, 243, 078,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia

Februari 2018 Wizara na Taasisi zake zilipokea **Shilingi Bilioni Themanini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Saba, Ishirini na Nane Elfu na Themanini na Tatu (86,977,028,083/=) sawa na asilimia 52%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimaimizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

## 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018,

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Elfu (23, 236, 830,000/=)** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** sawa na **Asilimia 77.46%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Ndani na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Elfu (5, 236, 830,000/=),** sawa na **Asilimia 22.54%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Laki Tano Hamsini na Sita Elfu (10,478, 556,000/=) sawa na asilimia 45.%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja na Tatu Elfu (9,261,003,000/=)**

sawa na **asilimia 51%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

### 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Ndani na Fedha hizo zimepatikana kwa wakati. Aidha, Ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya *MOLADI* ni mfumo wa gharama nafuu na unakamilisha ujenzi kwa haraka.

Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan Miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 23 na 24 Machi 2018. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainisha maeneo zaidi ya Arobaini (40) ya viapumbele kwa Taasisi zote zilizo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya kiwemo;

i) Kuanza Ujenzi wa Majengo ya Makao Makuu ya Mhimili wa Mahakama ya Tanzania Mjini Dodoma,

ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sheria,

iii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa kutenganisha mashtaka na Upelelezi,

iv) Kuweka Mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia, kuratibu mapitio ya Mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe,

v) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi mbalimbali chini ya Wizara na Taasisi zake,

vi) Kujenga na kuboresha Majengo ya Mahakama nchini,

vii) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria nchini,

viii) Kuwajengea uwezo Watumishi kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao, kuimarisha weledi na kuongeza tija,

ix) Kuimarisha Mfumo wa uandishi na urekebishaji wa Sheria,

x) Kukamirisha na kuboresha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na kufungua Ofisi katika Mikoa na Wilaya zilizoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,

xi) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi

xii) Kuchunguza Malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za Binadamu na ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora nchini,

xiii) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Sheria za Masoko ya Mazao ya Kilimo, Mfumo wa Sheria unaosimamia Ujenzi wa Nyumba Tanzania na Mfumo unaosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania

xiv) Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Wilaya na Mikoa nchini,

xv) Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu,

xvi) Kuongeza udahili wa Wanafunzi katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ili kuongeza idadi ya Wataalam wa Sheria nchini, na

xvii) Kuimarisha kurugenzi ya Mafunzo Endelevu ya Kimahakama na kuboresha Mitaala ya Stashahada na Astashahada ya Sheria katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa Taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano Saba Elfu na Mia Mbili (24,087,507, 200/=).** Kiasi hicho ni sawa na

Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Mafungu ambayo yamepanga kukusanya kiasi kikubwa cha Maduhuli kuliko Mafungu mengine, ni pamoja na **Fungu 40**(Mfuko wa Mahakama) ambao upo chini ya Kamati ya Bunge ya Bajeti na **Fungu 41**(Wizara ya Katiba na Sheria) ambayo imepanga kukusanya **Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Saba Hamsini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Mbili Elfu**
**(14, 753, 292,000/=)**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2**

**JEDWALI NA.2: Mpango wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka Wa Fedha 2018/2019**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,002,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 13,002,000 |
| 40 | Mfuko wa Mahakama | 12,328,200,862 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 14,753,292,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 0 |
| 59 | Tume ya Kurebisha Sheria | 150,000 |
| **JUMLA KUU** | | **24,087, 507, 200** |

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tano, Milioni Mia Saba Ishirini na Sita, Laki Saba Sitini na Tatu Elfu (145, 726,763,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Tano, Milioni Mia Mbili Tisini na Nane, Laki Moja Thelathini na Saba Elfu (75,298,137,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Sabini, Milioni Mia Nne Ishirini na Nane, Laki Sita Ishirini na Sita Elfu(70,428,626,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ni kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na.3.**

**Jedwali Na.3: Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MAOMBI YA FEDHA |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,097,343,000 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 8,964,382,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 4,171,217,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,955,105,000 |
| 40 | **Mfuko wa Mahakama (Kamati ya Bajeti)** | **141,584,739,000** |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 11,105,747,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 5,636,870,000 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 1,978,579,000 |
| **JUMLA KUU** | | **190,493,982,000** |

### 4.4 **Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Arobaini na Tano, Milioni Kumi na Tano, Laki Tano Themanini na Mbili Elfu (45,015, 582,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Kumi na Tano, Laki Tano Themanini na Mbili Elfu(27,015,582,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Fedha za Miradi ya Maendeleo imeongezeka zaidi ya **Shilingi Bilioni 21** ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 91%** ya Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kubaini ongezeko la Bajeti ya Maendeleo hatua ambayo inapongezwa, bado kiasi cha Fedha za Nje ni kikubwa ukilinganisha na bajeti ya ndani. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kupunguza utegemezi wa Fedha za Nje katika kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa kuwa upatikanaji wake unaweza usiwe wa uhakika na hivyo inaweza kukwamisha utekelezaji wa Miradi husika kwa wakati.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

### 5.1 FUNGU 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

i) **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Mahakama ni Chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Mahakama ya mwaka 2011. Jukumu la chombo hicho cha kiutawala ni kusimamia Mahakama ya Tanzania kama muhimili wa Serikali ambao umekuwa ukitekeleza kazi zake kwa uhuru na haki bila kuingiliwa na Chombo au taasisi nyingine yoyote kama ambavyo imetamkwa chini ya Ibara ya 107A na 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na malalamiko ya muda mrefu kuhusu changamoto mbalimbali katika usimamizi wa masuala mbalimbali ya kiutawala katika Mahakama, Serikali ilichukua hatua ya kufanya maboresho yaliyoanzisha Kada ya Watendaji wa Mahakama ambao wengi wao walikuwa Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, kwa lengo la kuisaidia Mahakama kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki kwa uhuru na kwa wakati**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwakuwa Kamati imebaini kuwa Watendaji hao wa Mahakama wameshindwa kuisaidia Mahakama kutatua kero zake, na kwakuwa imebainika kuwa Watendaji hao wamekuwa wakitumia nafasi zao vibaya kwa kutumia hata lugha zisizoridhisha, kujiingiza kwenye Maamuzi ya kesi wakati wao siyo Mahakimu wala Majaji, pia kuwanyanyasa Mahakimu na baadhi ya Majaji na hivyo kuathiri nia njema ya Serikali ya kuhakikisha Mahakama zinatumia rasilimali zilizopo katika kurahisisha utoaji haki kwa wakati,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, Serikali ione uwezekano wa kuiboresha Sheria ya Utawala wa Mahakama ili kuongeza udhibiti wa nidhamu za Watendaji hao hata ikibidi kuwarejesha kwenye nafasi zao za awali. Hatua hiyo italinda utambulisho na misingi ya asili ya Mahakama inayozingatia miiko na maadili ya kimahakama *(Judicial Identity).*

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wakati wa ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilibainika kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu Watumishi wengi wa Mahakama hususan Mahakimu kuhamishwa vituo vya kazi na kupandishwa vyeo bila kulipwa stahiki zao kwa wakati, Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatua changamoto hiyo kwa kuwalipa Watumishi wake wote ambao hawajalipwa stahiki zao katika Mahakama mbalimbali nchini.

iii) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na matumizi ya Teknolojia ya *MOLADI* katika ujenzi wa majengo ya Mahakama nchini, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe

kwa uwazi *(Transparent and Competitive Bidding Process)* na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya Wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha Miradi ya ujenzi wa Mahakama nchini kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

iv) **Mheshimiwa spika**, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka Paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya Sehemu za Paa hilo wakati Jengo hilo bado ni jipya. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kuokoa athari zinazoweza kujitokeza kwa Jengo ambalo limegharimu Mabilioni ya fedha.

v) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa mtiririko mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa Fedha za Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2018/2019), Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Tume ya Utumishi wa Mahakama zihakikishe fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika

kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(Value For Money).*

5.2 **Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini.

Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali na kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi wa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

5.3 **Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati ina shauri Ofisi hii iwe na rasilimali ya kutosha na iendelezwe ili kuimarisha uwezo wa Wanasheria wa Serikali katika

kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslai ya nchi.

## 5.4 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

i) **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa Ofisi hii, Kamati inashauri kuwepo kwa ushirikiano wa karibu katika kuratibu Mfumo mzima wa utoaji haki nchini baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi. Hatua hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii pamoja na kuongeza uwigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine vya kiupelelezi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Ofisi hii ihakikishe inafungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya zilizoainishwa katika taarifa ya Bajeti kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na Wananchi.

5.5 **FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu, ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa Watu magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha, Kamati ina shauri Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko hayo na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

5.6 **FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, imefanya maboresho makubwa ya Sheria mbalimbali nchini ikiwemo kutunga Sheria mpya zenye kugusa rasilimali za nchi katika Sekta mbalimbali nchini, Kamati inaishauri Tume ya kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mfumo wa Sheria nchini unaozungumza lugha moja *(Uniformity of Law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima *(unnecessary Conflict of Law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

## 5.7 FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshmiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, ilibainika kuwepo na upungufu wa idadi ya udahili wa Wanafunzi wa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Utumishi wa Mahakama imebainisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Mahakimu wa kutosha wenye kukidhi vigezo vya ajira katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya nchini. Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kuhakikisha inaboresha Mfumo wa udahili wa Wanafunzi ikiwemo kuona uwezekano wa kuanzisha matawi mbadala ya Taasisi hiyo na kuyaratibu kwa lengo la kuongeza uwigo wa udahili, ili kupata Wanasheria wa kutosha watakao tosheleza Soko la Ajira nchini.

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, hatua hiyo ihakikishe misingi ya kitaaluma inazingatiwa katika kuhakikisha Taasisi inazalisha Wanasheria wenye sifa stahiki ambao watakuwa na tija kwa Taifa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa Hekima na Weledi Mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba J.A.M Kabudi, (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam

wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. George Simbachawene, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
5. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-

14. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb- Mjumbe;
18. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard)

Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

18 APRILI, 2018